

## Maombi yanakubaliwa mwaka mzima.

Hati za kuthibitisha kuzaliwa na mapato zinahitajika kwa kila ombi.

Hali nyingine zinaweza kukidhi mahitaji ya ustahiki.

Miongozo ya mapato hutumiwa kutoka kwa miongozo ya hivi karibuni ya mapato ya shirikisho iliyotolewa.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali

Wasiliana nasi:

95 West 100 South Suite 200  
Logan, Utah 84321

(435) 755-0081

Hablamos Español

[www.brheadstart.org](http://www.brheadstart.org)



## Dhamira Yetu

Bear River Head Start imejitolea kutoa furasa za elimu na ukuaji kwa watoto, familia, wafanyakazi, na jamii katika mazingira ya kulea na kusaidia. BRHS itatimiza hili kwa uadilifu, heshima na uaminifu.



Bear River Head Start

HAWASAFIRISHI watoto kwenda au kutoka shulen.

Vibadala vya Usafiri:

- Mpango wa Nyumbani
- Wazazi wa Head Start wanaweza kuitumia usafiri wa pamoja
- Usafiri wa umma
- Wilaya ya shule hutoa usafiri kwa baadhi ya maeneo.

**Bear River**

**head**START

**Swahili**

Bear River Head Start ni mpanago wa wanawake wajawazito na watoto wa miaka 0-5, pamoja na wale wenye ulemavu.

Chekechea

Head Start ya Mapema

Huduma za Nyumbani



## Head Start ya Mapema

**Head Start ya Mapema huwahudumia wanawake wajawazito na watoto wenye umri wa miaka 0-3.**

Mpango wa Kituoni wa Head Start ya Mapema hutoa nafasi ya mapumziko kwa mtunzaji mkuu na huduma bora ya watoto kwa kina mama wajawazito na watoto hadi umri wa miaka mitatu. Kituo hiki kinafanya kazi kikiwa na uwiano wa watoto wanne kwa kila mwalimu. Kila mwalimu amefundishwa katika makuzi ya mapema ya mtoto ili kutoa kiwango cha juu zaidi cha utunzaji. Head Start ya Mapema huzingatia ukuaji wa watoto, uzazi/kushikamana, lishe, afya, na kutoa habari juu ya kusoma na kuandika, kuajiriwa, na kufikia malengo ya elimu.

Familia za watoto wachanga/watoto wadogo wenye ulemau au ucheleweshaji wa ukuaji hupokea huduma zilizoratibii na Watoa Huduma wa Part C.



Mipango ya Head Start ya Mapema na Head Start ya Chekechea, inatao Huduma za Nyumbani katika kaunti zifuatazo: **Box Elder, Cache, Rich, Bear Lake, Caribou, Franklin, Oneida na South Bannock**

## Head Start ya Chekechea

**Head Start ya Chekechea inahudumia watoto wenye umri kati ya miaka 3-5.**

Huduma za Kituoni zinaiga za darasani kwa watoto wa miaka 3 na 4 (mtoto lazima awe na umri wa miaka 3 ifikapo Septemba 1 ya mwaka wa sasa wa shule au awe na umri wa angalau miaka 3). Kila mtoto anachukuliwa kama mtu wa kipekee na anaruhusiwa kukua na kuendelea kwa kiwango chake mwenyewe. Watoto hukua, kujifunza, na kuendelea kupitia mazingira yaliyoboreshwa pamoja na wafanyakazi wanaojali ambao wanataka wafanikiwe. Kila darasa lina kati ya watoto 14 -18 (kulingana na ukubwa wa darasa) na mwalimu na msaidizi wa mwalimu. Madarasa huwa siku za Jumatatu - Alhamisi Unaweza kuchagua vipindi vyta asubuhi, mchana, na siku iliyoongezwa (masaa 6.5) kulingana na eneo.

## Nyumbani

Chaguo la mpango wa nyumbani limewekwa kwa misingi ya kwamba mzazi ndiye mwalimu wa kwanza na muhimu zaidi wa mtoto wake. Kujifunza hutokea kwanza nyumbani, mazingira ya asili zaidi. Wazazi daima wanafundisha! Kwa kuzingatia falsafa hii, familia zinazowaandikisha watoto wao katika mpango wa nyumbani zitapokea huduma za Head Start kupitia njia inayomzingatia mzazi. Huduma kwa watoto kimsingi ziko nyumbani kupitia ziara za nyumbani za kila wiki za Mwalimu wa Familia. Wazazi na watoto wanapewa fursa za kushiriki katika shughuli za kijamii.

Huduma za Bear River Head Start ni pamoja na:

- Chaguo za Kituo cha Chekechea, Kituo cha Head Start ya Mapema au Elimu ya nyumbani
- Msaada wa Ujauzito
- Mipango iliyobinafsishwa ya kujifunza
- Wakili wa familia anayesaidia mahitaji ya familia.
- Uchunguzi wa maendeleo
- Uchunguzi wa kusikia na kuona
- Milo yenye virutubisho
- Msaada wa afya ya akili

**Chaguo za Kituoni za Head Start ya Mapema:**

- ◆ Logan (South Center)  
670 West 400 South  
Logan, Utah 84321
- ◆ Logan (North Center)  
1300 North 200 East, Ste. 102  
Logan, Utah 84321

Masaa ya Head Start ya Mapema Jumatatu-Ijumaa 8:00 asubuhi -2:00 adhuhuri

**Chaguo za Kituoni za Head Start ya Chekechea:**

Logan, Brigham, Hyde Park, Hyrum, Malad, Richmond, Smithfield, Tremonton, Preston, Paris

